**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA VITUO VYA UWEZESHAWANANCHI KIUCHUMI KATIKA MIKOA NA HALMASHAURI ZA WILAYA


***Umeandaliwa na***
***Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)***
**12 Barabara ya Kivukoni**
**S.L.P. 1734, Dar-Es-Salaam**
**Simu: +255 22 2137362**
**Simu/Nukushi: +255 22 2125596**
**Barua Pepe: neec@uwezeshaji.go.tz**
**Tovuti: www.uwezeshaji.go.tz**



**MEI, 2019**

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **Halmashauri** | **:** Halmashauri ya Wilaya |
| **Kituo/Vituo** | **:** Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| **Taasisi** | **:** Taasisi zinazoshiriki kutoa huduma ndani ya Kituo |
| **NEEC** | **:** Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| **SACCOS** | **:** Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo |
| **OR TAMISEMI** | **:** Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **Mdau** | **:** Taasisi zote zinazoshiriki kuendesha na kutoa huduma katika Kituo |
| **NMSFEE** | **:** Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| **TIE** | **:** Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **NACTE** | **:** Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi |
| **TCU** | **:** Tume ya vyuo Vikuu |
| **VETA** | **:** Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| **TECC** | **:** Kituo cha Ushindani wa Kibiashara Tanzania |
| **IAE** | **:** Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| **ADEM** | **:** "Agency for Development of Education Management" |
| **TPB** | **:** Benki ya Posta Tanzania |
| **NMB** | **: "**National Microfinance Bank" |
| **UDSM** | **:** Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| **SUA** | **:** Chuo cha Sokoine cha Kilimo |
| **BODABODA** | **:** Pikipiki zinazotumika kutoa huduma ya usafiri kwa abiria |
| **PPRA** | **:** Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma |
| **VICOBA** | **:** Vikundi vya Akiba na Mikopo |
| **VICOBA FETA** | **:** Shirikisho la VICOBA Tanzania |
| **IR-VICOBA** | **:** Taasisi ya VICOBA vya Kidini |
| **TIMAP** | **: "**Tanzania Informal Microfinance Association of Practitioners" |
| **SIDO** | **:** Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo |
| **AGIFT** | **:** Mfuko wa Pembejeo wa Taifa |
| **MKURABITA** | **:** Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania |
| **TRA** | **:** Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **WDF** | **:** Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake |
| **TANTRADE** | **:** Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara |
| **YDF** | **:** Mfuko wa Maendeleo wa Vijana |
| **TCCIA** | **:** Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania |
| **NHIF** | **:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| **NSSF** | **:** Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |

**YALIYOMO**


VIFUPISHO VYA MANENO ..... 2
1.0. UTANGULIZI ..... 4
1.1. SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ..... 4
2.0. UTEKELEZAJI WA SERA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ..... 6
3.0. PROGRAMU ZA BARAZA ZA UWEZESHAJI WA VIJANA ..... 11
3.1. KIJANA JIAJIRI ..... 11
3.2. MAFUNZO KWA WAHITIMU WA VYUO VIKUU ..... 11
3.3. PROGRAMU YA BODABODA ..... 11
3.4. PROGRAMU YA VIJANA WA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) ..... 12
4.0. CHIMBUKO LA KUANZISHA VITUO VYA UWEZESHAJI NCHINI ..... 12
5.0. MWONGOZO WA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA KITUO ..... 13
6.0. MALENGO YA MWONGOZO ..... 13
7.0. WALENGWA WA KITUO ..... 13
8.0. UMUHIMU WA KUANZISHA KITUO CHA UWEZESHAJI ..... 13
9.0. UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KUANZISHA KITUO ..... 14
10.0. KAZI ZA KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ..... 15
11.0. MISINGI YA UTEKELEZAJI YA KITUO ..... 16
12.0. MUUNDO WA UTAWALA WA KITUO ..... 16
12.1. OFISI YA MKUU WA MKOA NA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA ..... 17
12.2. KAMATI YA MASHAURIANO YA MKOA AU WILAYA ..... 18
12.3. MAJUKUMU YATAASISI ZINAZOTOA HUDUMA KWENYE KITUO ..... 18
13.0. UTARATIBU WA KUGHARAMIA KITUO ..... 19
14.0. VYANZO VYA MAPATO KWA KITUO ..... 19
15.0. MATUMIZI YA FEDHA ZA KITUO ..... 19
16.0. UFUATILIAJI NA TATHMINI ..... 20
16.1. UFUATILIAJI NA TATHMINI ..... 20
16.2. TATHMINI YA KITUO KIMAKUNDI: ..... 20
17.0. KITUO CHA MFANO MKOANI SHINYANGA, WILAYA YA KAHAMA ..... 20
17.1. HISTORIA YA HALMASHAURI YA KAHAMA ..... 20
17.2. MCHAKATO WA UANZISHWA JI WA KITUO CHA KAHAMA ..... 21
17.3. USIMAMIZI WA KITUO CHA KAHAMA ..... 22
17.4. TAASISI ZINAZOSHIRIKI NDANI YA KITUO CHA KAHAMA ..... 22

## 1.0. UTANGULIZI

### 1.1. SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Kutokana na sababu za kihistoria, wananchi hawakushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi, kwa kuwa walinyimwa fursa. Hali hii ilikuwepo wakati wa ukoloni ambapo wananchi wengi waliwekewa vikwazo kushiriki katika uchumi. Wananchi walilazimika kujishughulisha na uchumi wa sekta isiyo rasmi wakati sehemu kubwa ya sekta rasmi ilishikwa na watawala wa kikoloni na wageni. Wakoloni walitumia mbinu mahsusi kuwaendeleza wazungu na wananchi wachache. Mbinu hizo ni pamoja na utoaji wa mikopo, utoaji wa elimu, ugawaji wa ardhi na utoaji wa leseni za biashara. Baadhi ya mbinu hizo zinaweza kutumika hivi sasa kurekebisha hali hiyo na kuwawezesha Wananchi kumiliki sehemu kubwa ya uchumi.

Baada ya uhuru mwaka 1961, Wananchi walipata madaraka ya kisiasa lakini sehemu kubwa ya uchumi bado ilibaki mikononi mwa wageni na baadhi ya Watanzania. Hali hiyo ilileta kero na ni mojawapo ya sababu muhimu ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, mwaka wa 1967. Azimio hilo lilikuwa ni mkakati muhimu wa kuhakikisha kwamba wananchi kwa pamoja kupitia dola wanashika njia kuu za uchumi. Shughuli zote za uzalishaji na utoaji wa huduma ziliundiwa mashirika ya umma. Hata hivyo, mashirika ya umma mengi yaliendeshwa kwa hasara na yaliendesha shughuli za kiuchumi kwa kutumia mtaji na ruzuku kutoka Serikalini.

Kabla na baada ya Uhuru kuna vyombo ambavyo viliongeza chachu ya wananchi kushiriki katika shughuli za uchumi. Kwanza ni Vyama vya Ushirika hasa katika uzalishaji, utoaji mikopo ya pembejeo, huduma za ugani na masoko ya mazao kadhaa kama vile pamba na kahawa. Pili, ni Serikali za Mitaa ambazo zilikuwa na uwezo wa kuwashirikisha kwa karibu wananchi katika shughuli za uchumi. Aidha, katika mwaka wa 1973 Serikali ilianzisha Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kwa ajili ya kuendeleza viwanda vidogo nchini.

Mchango wa SIDO katika kuendeleza viwanda vidogo vinavyoendeshwa na wananchi umekuwa mkubwa kwa kutumia mbinu za mafunzo, ushauri na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu. Hata hivyo, mafanikio yake yangekuwa makubwa zaidi kama shughuli za SIDO zingekuwa zimetekelezwa chini ya mwongozo wa Sera ya Uwezeshaji. SIDO haikuweza kutekeleza wajibu wake kikamilifu kutokana na kutokupata fedha za kutosha kuendeshea shughuli zake.

Mwaka wa 1992, Sera ya Ubinafsishaji ilianzishwa baada ya kuona kwamba mashirika ya umma yalikuwa mzigo kwa Serikali ambayo haikuwa na fedha za kuyaendesha na kuyaendeleza hata kufikia uamuzi wa kuyerekebisha na mengine kuyabinafsisha. Sehemu kubwa ya wanachi haikushiriki ipasavyo katika zoezi la ubinafsishaji kwa kuwa hawakuwa na elimu ya biashara, ujuzi na mitaji. Aidha, utaratibu wa kuanzisha Amana ya Ubinafsishaji (Privitization Trust) kwa ajili ya kusaidia wananchi kushiriki kununua hisa katika mashirika ya umma yaliyokuwa yamebinafsishwa haukutekelezwa, sababu mojawapo ikiwa, ni kutokuwepo kwa Sera ya Uwezeshaji. Serikali kwa kuzingatia yote haya,iliamua kuwe na Sera ya Uwezeshaji wananchi

kiuchumi ambayo ndiyo mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wa wananchi katika sekta zote.

Walengwa wa Sera ya Uwezeshaji ni wananchi. Makampuni ya wananchi ni yale ambayo yamesajiliwa Tanzania ambayo walengwa wanamiliki asilimia isiyopungua hamsini ya hisa zote za makampuni hayo. Sera ya uwezesahji inajumuisha wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyakazi na wafanya biashara katika sekta mbali mbali na makundi mengine. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji inatoa mwongozo unaotafsiri uwezeshaji unavyotakiwa kuwa katika sehemu mbali mbali kulingana na mazingira ya sekta husika.

Ushiriki wa wananchi wengi katika shughuli za uchumi wa kisasa ni duni. Sehemu kubwa ya uchumi huo imeshikwa na wageni au Watanzania wachache. Hali hiyo inapingana na dhana ya kuleta maendeleo yanayonufaisha na kutoa nafasi ya maendeleo kwa wananchi wengi. Wengi wao wameshindwa kushiriki kwa sababu ya uwezo mdogo kimtaji, ukosefu wa ujuzi na uzoefu wa biashara pamoja na matatizo yanayohusiana na kutokukopesheka.

Sera ya Uwezeshaji inalenga kuondoa vikwazo vya wananchi kushiriki kwenye uchumi wan chi yao ili kutoa nafasi nzuri zaidi kwa makundi mbali mbali kushiriki kikamilifu zaidi katika shughuli za uchumi.

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeandaliwa kwa kuzingatia nguzo tisa ambazo zikitekelezwa kwa ukamilifu zitawezesha watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa nchi.

1. Uboreshaji wa mfumo wa utawala wa kodi, sheria, kanuni, leseni na huduma nyingine za serikali.
2. Kukuza mitaji
3. Kukuza uchumi wa mazingira bora ya uwekezaji
4. Matumizi bira ya ardhi
5. Uimarishaji wa masoko na ubia
6. Wananchi kunufaika na ubinafsishaji na hisa
7. Miundombinu ya kiuchumi
8. Kuinua viwango vya elina na ujuzi
9. Kuimarisha ushirika nchini

Nguzo za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kichumi ya Mwaka 2004 zinaelekeza kuwa kila Wizara, Idara na Wakala wa Serikali ni watekelezaji wa Sera. Baraza ni chombo kilichoundwa kusimamia utekelezaji wa sera hii na limepewa mamlaka hayo kwa Sheria ya Uwezeshaji Na. 16 ya 2004. Kazi kubwa ya Baraza ni kuandaa Mikakati na Miongozo ya Uwezeshaji ya kitaifa inayohusisha sekta mbalimbali katika ngazi zote za kiutawala/kisera. Hivyo Baraza ni chombo cha uongozi na uratibu wa utekelezaji wa sera ya uwezeshaji

kwakusimamia, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji kulingana na Sera, Sheria, Mikakati na Miongozo ya uwezeshaji iliyopo.


Moja ya mafanikio makubwa kabisa ni kuandaliwa kwa mkakati wa sekta mbalimbali wa utekelezaji wa sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na mwongozo wake, ambao pia umeelekeza mfumo wa uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuanzia ngazi ya kitaifa mpaka ngazi ya vijiji ambapo kamati mbalimbali za uwezeshaji hukaa kujadili masuala ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

## 2.0. UTEKELEZAJI WA SERA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limepewa mamlaka ya kuandaa Mikakati na Miongozo ya Uwezeshaji ya kitaifa inayohusisha sekta mbalimbali katika ngazi zote za kiutawala/kisera. Moja ya Mikakati hiyo ni Mkakati waTaifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (National Multisectoral Strategic Framework for Economic Empowerment- NMSFEE).

Utekelezaji wa Mkakati unafanywa na Wizara na Taasisi zake; Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ikihusisha mikoa na Halmashauri katika ngazi zote; SektaBinafsi pamoja na Wadau wa Maendeleo. Mkakati huu unatekelezwa kupitia Mwongozo ulioandaliwa ili kutoa maelekezo ya namna ya kutekeleza Mkakati huo. Huu ni Mwongozo wa kitaifa kwa ajili ya kuwezesha uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji waSera katika ngazi na sekta zote za kiuchumi kupitia Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji WananchiKiuchumi. Mfumo wa uratibu wa uwezeshaji umepangwa kwa kuwa na kamati kuanzia ngazi ya Taifa hadi kijiji/mtaa na kila kamati ikiwa na majukumu yake kwa mtiririko endelevu.

Mfumo wa juu kabisa katika uratibu ni Mkutano wa Mwaka wa Uwezeshaji ambao unafanyika kila mwaka chini ya Mwenyekiti ambaye ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mkutano huo unafuatiwa na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya uwezeshaji chini ya mwenyekiti ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu). Kamati ya Ushauri inapokea taarifa za utekelezaji kutoka kamati za kitaalam za Kisekta, Ushiriki wa Watanzania katika Uwekezaji, Vikundi vya Kijamii, Mifuko ya Uwezeshaji, na Ujasiriamali. Aidha, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinaratibu masuala ya uwezeshaji kupitia kamati zilizopo kisheria na zinasaidiwa na waratibu wa uwezeshaji wa Mikoa na Halmashauri.




***Mchoro 1: Mfumo wa Uratibu wa Uwezeshaji***

Wizara, Mikoa 26 ya Tanzania Bara na Halmashauri 185 zimeteua Waratibu wa Dawati la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, vilevile Wizara zote zimeunda kamati za kusimamia na kuratibu masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Uteuzi huu unaleta matumaini makubwa ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa mtanzania mmoja mmoja kutokana na kila sekta, mikoa na halmashauri kutekeleza na kuhuisha uwezeshaji kama sehemu ya shughuli zao za kila siku.

Utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umekuwa wa mafanikio sana hapa nchini. Hii inatokana na kwamba Sera nyingi za kiuchumi sasa hivi zimebeba matamko ya kiumwezesha mtanzania kiuchumi. Vilevile sheria nyingi zimeelekeza uwezeshaji wa watanzania katika utekelezaji wake. Vilevile utekelezaji wa uwezeshaji wa wananchi unafanyika katika makundi yote ya kijamii. Ikiwa utekelezaji sasa hivi unafanyika na sekta ya umma na sekta binafsi, zikiwemo Assai za Kiraia.


Vilevile waratibu wanaosimamia ushiriki wa watanzania katika miradi ya serikali na uwekezaji (Local Content) waliteuliwa kutoka kwenye Wizara na taasisi za Serikali ambapo kati yao 29 wanatoka kwenye Wizara na 26 ni katika taasisi za Serikali.Majukumu ya waratibu hao pamoja na mambo mengine ni pamoja na kufuatilia ushiriki wawatanzania katika sekta zao, kuwasilisha taarifa ya ushiriki wa watanzania katika ofisi za Baraza,kufanya mapitio ya Sera na Sheria zao ili kuhakikisha suala la ushiriki wa watanzania katikasekta zao linapewa kipaumbele na kuhakikisha watanzania wanashiriki kikamilifu katika miradi mikubwa ya uwekezaji

inayofanyika hapa nchini.

Kamati za kisekta zimeundwa ambazo zitajadili kwa kina fursa, changamoto na kuweka mipango madhubuti ya kuongeza ushiriki wa watanzania katika sekta mbalimbali. Kamati hizo ni kama zifuatazo:

1. Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi,
2. Kamati ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano,
3. Kamati ya Madini, Mafuta na Gesi
4. Kamati ya Viwanda, Biashara na Utalii
5. Masuala ya Fedha, Bima, Ununuzi, Elimu na Ajira ni mtambuka

Kamati hizi zinaripoti kwenye Kamati ya Kitaifa ya Ushiriki wa Watanzania Katika Uwekezajikatika Sekta mbalimbali (National Multi Sector Local Content Committee) ambayo inawajumbe kutoka sekta za Umma na Binafsi na Mwenyekiti wake ni Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.




***Mchoro 2: Mfumo wa Uratibu wa Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji***

Utekelezaji wa masuala ya ushiriki wa watazania kwenye uwekezaji na miradi yote ya Serikali umeshika kasi sana sasa hivi. Hii imechochewa na baadhi ya Sera na Sheria kuwa na maelekezo maalumu kuhusu ushiriki wa watanzania. Baadhi ya sheria ni pamoja na sheria ya mafuta na gesi, madini, huduma ndogo za fedha, bima na manunuzi ya umma.

Ujasiriamali ni moja ya nguzo tisa za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji ambayo ni kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu ili kuendeleza ujasiriamali. Tamko la Sera ni kuangalia upya mfumo wa elimu ili kujenga wananchi wenye kujiamini, wabunifu na ari ya kuzalisha mali ambapo mkakati wa sera unalenga kurekebisha mitaala ya elimu ili kutoa elimu na ujuzi wa ujasiriamali ili

kukidhi tamko la Sera. Hii inatokana na changamoto za kimkakati ambazo zimedhihirisha kuwa wadau wengiwamekuwa wakitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa kutumia miongozo ambayo haiko sawa; na hakunamaafikiano kuhusu uelewa wa pamoja wa dhana nzima ya ufundishaji ujasiriamali, madhumuniyake, matarajio yanayotazamiwa kufikiwa na mwanafunzi. Ili kuondokana na changamoto zaujasiriamali Baraza kwa kushirikiana na wadau wa elimu na mafunzo ya ujasiriamali kama vile Taasisi ya Elimu Tanzania (**TIE**), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (**NACTE**), Tume ya Vyuo Vikuu(**TCU**), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (**VETA**) liliandaa Mwongozo wa Taifa waUfundishaji Ujasiriamali kwa lengo la kubainisha matarajio ya msingi kwa mwanafunzi baadaya kujifunza ujasiriamali, njia za kufundishia, mwongozo wa ubora kwa wawezeshaji na mbinu za upimaji ujuzi wa mwanafunzi zitakazotumiwa kwenye ufundishaji ujasiriamali. Lengo kubwani kuhakikisha jitihada za ujasiriamali zinachangia kwa ufanisi zaidi kuwawezesha Watanzaniakuboresha mitazamo, maarifa na ujuzi wao.Utekelezaji wa Mwongozo huu umeleta mafanikio mbalimbali ikiwemo kuwezesha matumizi rasmiya Mwongozo huo kwa waandaaji na wathibiti wa mitaala nchini (**TCU**, **NACTE**, **VETA, TIE**, **IAE**, **ADEM**) kwa kuingiza ujasiriamali katika mitaala na kujengea uwezo kwa vijana na kuendeleza biasharakupitia programu za mafunzo mbalimbali ikiwemo mitaji yenye masharti nafuu na malezi ya biashara.Aidha, ili kuimarisha uongozi na uratibu wa ujasiriamali nchini, Kamati ya Kitaifa ya Maendeleo ya Ujasiriamali (National Entrepreneurship Development Committee) inayowajumuisha wajumbe kutoka katika sekta ya umma, taaluma na binafsi imeundwa na hukutana mara mbili kwa mwaka. Kamati hii inaleta pamoja utaalam wa ujasiriamali ili kuimarisha ujasiriamali na kushauri fursa za kijasiriamali zenye tija.

Baraza kwa kushirikiana na wadau liliandaa Mkakati wa Taifa wa Ujasiriamali ambao umejikita katikamaeneo muhimu yaliyofanyiwa utafiti ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaimarisha ujasiriamali. Maeneo hayo ni pamoja na kukuza ujuzi wa wajasiriamali, kukuza ushirikiano na mtangamano, Kukuza ubunifu na teknolojia, kuongeza upatikanaji wa mitaji na huduma za kifedha na kuboresha mazingira ya kisheria. Katika hatua nyingine pia Baraza limetengeneza mwongozo wa kiongozi cha kufundishia Ujasiriamali kwa wajasiriamali walio nje ya mfumo wa elimu. Hatua hii imefikiwa ili kuboresha elimu inayotolewa kwa wajasiriamali hapa nchini na kutoa mwongozokwa walimu wanaofundisha. Mwongozo huu umezingatia biashara ndogo, za kati na biashara kubwa. Utengenezaji wa mwongozo ulihusisha kupata kanzidata za waalimu wote wanaofundisha maendeleo na huduma za biashara hapa nchini, ambao pia walishiriki kutoa maoni. Sekta ya biashara ndogo na za kati imekuwa ikikumbana na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa huduma bora za maendeleo ya biashara. Watoa huduma hizo hawana mfumo rasmi wa kuwaratibu ili kuhakikisha ubora wa huduma wanazotoa sambamba na kutambua mahitaji na idadi halisi. Baraza linaratibu utambuzi wa watoa huduma hao ili kuweza kuandaa kanzi data ya watoa huduma. Serikali inahimiza watoa huduma wote wa kuendeleza sekta ndogo na kati waweze kujisajili Baraza ili kuweza kutambuliwa.

Baraza la Uwezeshaji linaratibu Mifuko na Programu za Uwezeshaji 46 ambazo zimegawanyika katika makundi makuu manne nayo ni mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja kwa wananchi, mifuko inayotoa dhamana kwa kupitia benki za biashara, mifuko inayotoa ruzuku na mifuko inayoongeza ukwasi kwenye benki za biashara ambazo zimekuwa hazipendelei kutoa mikopo kwenye baadhi ya maeneo au sekta kama vile kilimo au nyumba nafuu. Aidha mifuko hii ilianzishwa kutatua changamoto mbalimbali zilizoonekana ikiwa ni pamoja na ufinyu wa vyanzo vya akiba kwa wananchi kutokana na kipato kidogo na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba; ukosefu wa dhamana zinazohitajika na benki; ukosefu wa utambulisho rasmi; kutokuwa na chombo cha kusimamia kumbukumbu za wakopaji; ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka na ukosefu wa mitaji wa kuchangia uanzishaji wa miradi. Walengwa wakuu wa mifuko ni wananchi wote wakiwemo wale wenye kipato kidogo, chakati na kikubwa, vikundi ama makampuni yaliyoko katika Sekta zote za kiuchumi. Baraza liliunda kamati ya kitaifa (National Economic Empowerment Funds Committee) ambayo huikutanisha mifuko yote ya nchi nzima mara mbili kwa mwaka.

Baraza linashirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ili kutekeleza mpango wa ushiriki wa makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye manunuzi ya umma. Katika mpango huu, sheria ya manunuzi imefanyiwa marekebisho ili kukidhi ushiriki wa makundi hayo. Mwongozo wa utekelezaji umeandaliwa na kusambazwa kwa Maafisa Masuuli ili waweze kutekeleza vizuri mpango huo. Mpango wa mafunzo kwa makundi maalumu na watendaji wa Serikali unaendelea kufanyika ili kurahisisha utekelezaji.

Mojawapo ya majukumu ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama yalivyoainishwa kwenye Sera ya Uwezeshaji ni kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo (**SACCOS**) na vikundi vya wananchi vya kuweka akiba na kukopa (k.m. **VICOBA** ,**VSLA**, **SILK n.k**.). Baraza limeweza kufanya jitihada katika kuuwezesha mfumo wa **VICOBA** kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na katika mazingira yanayoeleweka. Baraza limeweka mfumo wa kufanya vikao mara mbili kwa mwaka kwa lengo la kusimamia shughuli za **VICOBA** nchini. Baraza limesaidia uanzishwaji na usajili wa taasisi miavuli za **VICOBA-FETA** kama (umbrella organization) yenye jukumu la kuziunganisha asasi/taasisi zinazojihusisha na **VICOBA;** na kuwa chombo cha majadiliano na Serikali kuhusu maendeleo ya VICOBA nchini. Mpaka sasa taasisi miavuli za **VICOBA** ziko tatu ambazo ni **VICOBA FETA** ambayo ni mwavuli wa asasi za kitanzania zinazosimamia **VICOBA, IR VICOBA** ambayo ni mwavuli wa asasi za kidini zinazosimamia **VICOBA** na **TIMAP** ambayo ni mwavuli wa asasi za kimataifa zinazosimamia **VICOBA** na vikundi vingine.

## 3.0. PROGRAMU ZA BARAZA ZA UWEZESHAJI WA VIJANA

Baraza limekuwa likitekeleza Programu mbalimbali kwa ajili ya kuleta mwamko kwenye eneo husika au kusaidia wananchi kwenye suala hilo. Programu hizi ni pamoja na programu za vijana (Kijana Jiajiri, JKT, Young Graduate programs), programu za wanawake na utekelezaji wa programu ya ushiriki wa watanzania kwenye uwekezaji na miradi ya serikali ya kimkakati.

### 3.1. KIJANA JIAJIRI

Programu hii inasimamiwa na Baraza na kutekelezwa na *Tanzania Enterpreneurship Competitive Centre* (**TECC**) – Asasi ya Kiraia iliyoanzishwa kwa ushirikiano wa Serikali na Sekta Binafsi. Programu hii inalenga vijana wa umri wa miaka 18-35. Ilianza kwa majaribio mwaka 2015 katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Dar es salaam. Mpaka sasa imefikia vijana 2000 ambapo utekelezaji wa Programu hufanyika kwa kutoa mafunzo ya wiki 6 ya biashara na ujasiriamali ambapo mafunzo hutolewa na **SIDO**. Vilevile vijana huwekwa kwenye malezi ya biashara kupitia wafanyabiashara wazoefu (wanachama wa **TCCIA**) kwa mwaka mmoja. Programu ya majaribio ilifikia mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Morogoro. Baada ya Majaribio ya mwaka mmoja, Programu hii imeendelea katika mikoa ya Mtwara, Dar Es Salaam, Pwani na Dodoma ambapo sasa hivi inajumuisha mafunzo ya Ujasiriamali, Malezi, Upatikanaji wa Mitaji na Stadi za Maisha. Mafunzo ya Stadi za Maisha yanatolewa na **VETA**. Program hii imekuwa ikitekelezwa kwa msaada wa fedha kutoka Youth Business International, **LNG** Consortium of Companies, Barclays, International Youth Foundation and MasterCard Foundation.

### 3.2. MAFUNZO KWA WAHITIMU WA VYUO VIKUU

Baraza limekuwa likiendesha Programu ya vijana waliomaliza vyuo vikuu na ambao bado wanasoma. Programu hii imekuwa ikitekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam na wadau mbalimbali. Programu hulenga vyuo vikuu vyote nchini na hutoa mafunzo ya wiki 8 ya biashara na ujasiriamali, ambapo vijana wanaandika wazo la biashara na kushindanishwa. Mpaka sasa vyuo vilivyoshiriki ni pamoja na UDSM, Ardhi, SUA na Muhimbili. Programu imekuwa ikisaidiwa na wadau ambao ni Ubalozi wa Uholanzi, Smart Villages, Anglo Gold, Benki ya **TPB, NMB** na **UTT MFI** na jumla ya vijana 143 wamenufaika na program hiyo ambapo wameanzisha na kuendesha biashara mbalimbali zikiwemo kilimo, ufugaji, utengenezaji wa bidhaa mbalimbali pamoja na kutoa ushauri wa biashara.

### 3.3. PROGRAMU YA BODABODA

Baraza kwa kushirikiana na mikoa linatekeleza programu ya uwezeshaji kwa vijana wa Bodaboda. Programu hii inalenga kuratibu na kuboresha maisha ya vijana wa bodaboda kiuchumi kwa vijana wanaoendesha bodaboda nchini. Lengo ni vijana kuanzisha **SACCOS** zao ambazo zitawawezesha kuweka akiba na kuanzisha shughuli mbadala za kiuchumi ambazo zitawaongezea kipato na kuanzisha miradi mikubwa zaidi. Baraza linalenga kuwa na **SACCOS** za **BODABODA** kila Mkoa ambapo **SACCOS** zitatakiwa ziwe na programu za kuboresha

uchumi. Sasa hivi Baraza linaandaa mwongozo ambao utatolewa kwa mikoa yote nchini kuhusu utaratibu wa kuviwezesha vikundi vya vijana wa Bodaboda.

### 3.4. PROGRAMU YA VIJANA WA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT)

Baraza kwa kushirikiana na JKT linatekeleza programu ya vijana wanaoingia JKT. Ambapo mwaka 2015 Baraza liliingia makubaliano ya miaka 5 ya kufundisha wakufunzi wote wa JKT ili nao wafundishe vijana ambao wanaingia JKT kuhusu biashara, ujasiriamali na ushirika wa kuweka akiba. Hivyo mafunzo ya wiki 2 yalitolewa kwa walimu wote wa JKT pamoja na viongozi wote wa kambi za JKT. Kuanzia mwezi Disemba 2017 vijana waliootoka JKT ni wale waliopatiwa mafunzo ya biashara na ujasiriamali ikiwemo uanzishaji wa vyama vya ushirika na vikundi vya kiuchumi. Programu hii inafikia vijana 7,000 kwa mwaka ambapo vijana wanapomaliza wanaunganishwa na vyombo vya fedha kwa mikopo nafuu kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na kuwezeshwa kushiriki katika shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi kibiashara ili kujiongezea kipato na kujitegemea.

## 4.0. CHIMBUKO LA KUANZISHA VITUO VYA UWEZESHAJI NCHINI

Chimbuko la kuanzishwa kwa vituoMaalum vya Kuhudumiawananchi na wajasiliamali ni matokeo ya utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kasimu M. Majaliwa (Mb), ambaye alifanya ziara mkoani Shinyanga na baadae kwenye wilaya ya Kahama. Akiwa wilayani Kahama alitambua mchango wa uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Shinyanga hususan Halmashuri ya Mji wa Kahama kwa kuchukua jitihada ya kutenga na kugawa maeneo ya kufanyia shughuli za uzalishaji kwa Wajasiriamali. Mhe. Waziri Mkuu alitembelea Halmashauri ya Mji wa Kahama na kubaini kuwa katika eneo la Bukondamoyo kumetengwa eneo la ekari 500 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogovidogo vya Wajasiriamali hasa vijana na wanawake. Katika eneo hilo viwanja 623 vimepimwa, kutolewa hati na kugawanywa kwa Wajasiriamali wazalishaji ili viwanja hivyo viweze kutumika kwa shughuli za uzalishaji na biashara nyingine ikiwemo kuweka mashine za kupasua mbao, useremala, uzalishaji, kuchomea vifaa mbalimbali (Welders), biashara za huduma na kufanya biashara ndogondogo.Aidha, katika eneo hilo Wajasiriamali 1,021 (wengi wao wakiwa ni vijana na wanawake) walipewa viwanja kulingana na shughuli wanazofanya.

Baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuona jitihada kubwa zilizofanyika wilayani Kahama, alitoa agizo kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (**NEEC**) lianzisheKituo Maalum cha kuhudumia wananchi kwenye masuala yote ya kiuchumi wakiwemo wajasiriamali, wakulima n.k. ambapo kituo hicho kinategemewa kuwa ni kituo cha mfano kwa Halmasahuri zote nchini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza kwamba baada ya kuanzishwa kituo cha Kahama. Baraza liandae mwongozo ambao yeye atautoa kama maelekezo ya kuanzisha vituo hivyo nchi nzima.

## 5.0. MWONGOZO WA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA KITUO

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kutoa maelekezo na maelezo kuhusu uanzishaji, uendeshaji, usimamizi na uratibu wa Kituo ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi na wajasiriamali kwa ufanisi.

Huu utakuwa ni mwongozo kwa Mikoa yote na Wilaya au Halmashauri mbalimbali hapa nchini ili ziweze kufaninikisha na kuendesha vituo vya uwezeshaji ambavyo vitasaidia utaekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kwa nchi nzima.

## 6.0. MALENGO YA MWONGOZO

Malengo ya mwongozo huu ni kutoa mwelekeo wa uanzishwaji na uendeshwaji wa kituo cha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kuwezesha Wananchi kupata huduma kwa urahisi katika eneo moja. Lengo ni kusaidia upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi ambapo mjasiriamali atapata huduma zote muhimu kituoni hapo. Pamoja na lengo kuu hilo yafuatayo pia ni muhimu katika utekelezaji wa shughuli za kituo:

i. Kuimarisha utendaji wa Taasisi zinazotoa huduma za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi;
ii. Kuainisha majukumu na wasimamizi wa Kituo katika kila ngazi;
iii. Kusimamia uendeshaji na utawala wa Kituo;
iv. Kufafanua mfumo au muundo wa utekelezaji wa majukumu na utoaji wa taarifa kwa kila mdau.

## 7.0. WALENGWA WA KITUO

Walengwa wanaotarajiwa kunufaika na kituo ni wananchi na wajasiriamali wote wakiwemo wadogo, wakati na wakubwa, Vikundi na Makampuni yaliyopo katika Sekta zote za kiuchumi.

## 8.0. UMUHIMU WA KUANZISHA KITUO CHA UWEZESHAJI

Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni juhudi za makusudi zinazoanzishwa na Serikali ili kuwasaidia wananchi wake waweze kushiriki vizuri katika shughuli za kiuchumi. Uwezeshaji unaweza kufanyika kwa kupitia Sera sahihi, Sheria sahihi, kukuza ujuzi wa wananchi, upatikanaji wa mitaji nafuu, taarifa sahihi za masoko na programu mahsusi ambazo zinazompa fursa mwananchi ya kushiriki vizuri kwenye uchumi. Watanzania wengi sana wanahitaji kupata taarifa, elimu, ujuzi na mitaji ili kuweza kusonga mbele kwenye juhudi zao za kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Uanzishwaji wa kituo cha uwezeshaji ni utaratibu muafaka ambao utaondoa adha ya watanzania katika kutafuta taarifa, elimu na ujuzi kwenye maeneo ya biashara na mambo mengine ya kiuchumi, kufahamu taratibu za urasimishaji wa biashara, taarifa za masoko, kuongeza thamani ya mazao, kufahamu fursa za hifadhi ya jamii, kupata elimu ya kodi na kufahamu fursa za mitaji.

Kituo cha Uwezeshaji ni nyenzo muhimu ambayo itafanya baadhi ya Taasisi za Serikali za kitaifa ambazo zinatoa huduma mbalimbali kupata urahisi wa kuwafikia wananchi kwa kupitia vituo hivi. Hivyo Mikoa yote ya Tanzania inasisitizwa kuanzisha vituo hivi ili kuwezesha upelekaji wa huduma kwa wananchi kwa urahisi.

Kabla ya kuanzishwa kwa kituo cha uwezeshaji wananchi hawata kuwa na mahala popote ambapo wanaweza kwenda kuuliza kama wana maswali yoyote. Vilevile kwa mwananchi ambaye hana taarifa kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na serikali, akifika kituoni hapo ataelewa kwamba kuna mambo mengi na huduma ambazo hapo awali alikuwa hajui.

Kituo cha uwezeshaji ni tofauti na vituo vingine ambavyo vimewahi kuanzishwa, kwa sababu lengo lake kubwa ni kumwendeleza mwananchi kiuchumi kwa kuleta huduma zote za serikali na sekta binafsi katika eneo moja. Lakini pamoja na huduma hizo pia kituo kitamjengea uwezo mwananchi kielimu, kiujuzi, kitaarifa na kifedha. Hivyo inategemewa kwamba kituo kitakapoanza kitaboresha huduma kwa wananchiUkuaji na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kwa wananchi; na Kuongezeka kwa Ajira.

## 9.0. UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KUANZISHA KITUO

Mikoa yote kupitia Halmashauri zilizomo ndani ya mkoa itaanzisha vituo vya uwezeshaji. Mkoa unaweza kutumia Halmashauri moja au zaidi kuweka vituo hivi. Mkoa au Halmashauri itatenga jengo au eneo ambalo litatumika kwa ajili hiyo.Mkoa au Halmashauri utaainisha aina ya huduma zinazohitajika na aina ya taasisi itakayotoa huduma hizo. Itakuwa vyema kama Mkoa au Halmashauri itashirikiana na NEEC katika kukubaliana taasisi ambazo zitakuwa zinatoa huduma katika kituo hicho, lakini pia ubunifu wa Mkoa unahitajika. Taasisi zinazotoa huduma zifuatazo zitafaa kutoa huduma zake hapo kituoni:-

a) Urasimishaji wa biashara (leseni, msimbomilia, vibali vya viwango vya bidhaa na chakula)
b) urasimishaji ardhi,
c) elimu ya kodi,
d) elimu ya ufundi,
e) elimu ya kuongeza thamani bidhaa,
f) Huduma za kibenki,
g) mikopo nafuu,
h) bima ya afya,
i) hifadhi ya jamii,
j) taarifa za masoko na mtandao wa masoko,
k) elimu kwa ujumla,
l) elimu ya uanzishwaji wa vyama vya ushirika,
m) elimu kuhusu vikundi vya kijamii n.k.

Kituo cha uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Kihama kitakuwa ni kituo cha mfano kwa Halmshauri zote Tanzania Bara, aidha hatua ya uanzishwaji wa Vituo kwa mikoa na halmshauri nyingine mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:-

i. Mahitaji ya wananchi ya huduma za uwezeshwaji
ii. Uwepo wa Shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa katika Hamashauri hiyo

iii. Madhumuni makuu ya uanzishwaji wa Kituo
iv. Kuwa na Jengo la kutolea huduma litakalofikika kwa urahisi na wananchi
v. Uchaguzi wa watoa huduma watakao kamilisha madhumuni ya kituo kulingana na mahitaji ya wananchi
vi. Uandaaji wa Mwongozo rahisi wa kuendesha kituo
vii. Kuandaa andiko litakaloainisha maeneo ya uwekezaji

## 10.0. KAZI ZA KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kinaanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma kwa wajasirimali na wananchi kwa ujumla ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha ama kuendeeza biashara na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kituo kinawakutanisha wadau mbalimbali wa uwezeshaji katika eneo moja ili waweze kutoa huduma kwa walengwa.Kituo hiki kitamrahisishia mwananchi kupata huduma za uwezeshaji katika eneo moja kwa mujibu wa malengo ya kituo kama yalivyoainishwa. Pia wasimamizi wa Kituo watakuwa na jukumu la kuandaa taarifa ua Uwezeshaji na kuiwasilisha kwenye mamlaka zinazohusika kwa ushauri na maamuzi.

Kituo kitafanya mambo yafuatayo:

a) Kutoa huduma za elimu na ujuzi mbalimbali
b) Huduma za kurasimisha biashara kama vile leseni na vibali vyote vinavyohitajika kama vile vibali vya shirika la viwango, mamlaka ya chakula na dawa, kurasimisha ardhi, huduma za msimbomilia
c) Huduma za kibenki na mikopo
d) Elimu ya kodi,
e) Elimu ya ufundi,
f) Elimu ya kuongeza thamani bidhaa,
g) Huduma za mikopo nafuu ya serikali kutoka kwenye mifuko ya serikali,
h) Huduma za bima ya afya,
i) Huduma za hifadhi ya jamii,
j) Elimu kwa ujumla,
k) Elimu ya vyama vya ushirika,
   Wasimamizi wa kituo pia watachukua takwimu za idadi ya wananchi wanaohudhuria kwenye kituo
   Taarifa zitakazokusanywa pia zitajumuisha mahitaji ya wananchi ambayo kwa sasa huduma zake hazitolewi.
l) Elimu ya uanzishwaji wa vikundi vya kijamii n.k.
m) Kituo kitatoa huduma za maeneo ya kufanyia aina mbalimbali za biashara kutokana na ukubwa wa eneo la kituo na mazingira husika.
n) Huduma za masoko na kutengeneza mtandao wa masoko.

## 11.0. MISINGI YA UTEKELEZAJI YA KITUO

Kituo cha uwezeshaji wananchi Kiuchumi ni eneo maalum lilitengwa na serikali kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi kwa utaratibu wa tofauti kidogo na ule wa kawaida. Taratibu zote za uendeshaji wa kituo zitazingatia sheria na taratibu za serikali lakini pia wadau wengine wanaosaidia wananchi kutoka sekta isiyo ya serikali wanaweza kukaribishwa kuungana na serikali katika kutoa huduma. Matumizi ya ofisi yanaendana sambamba na malengo na kazi zakuanzishwa kwa kituo. Haitaruhusiwa kuwa na mengine nje ya madhumuni yaliyopelekea kuanzishwa kwa kituo hiki.

Ifuatayo ni misingi ya uendeshaji wa kituo cha uwezeshaji wa wa wananchi kiuchumi hapa nchini:

(i) Kituo kitafuata mahitaji ya mkoa au halmashauri au hata kanda husika ili kukidhi mahitaji na matakwa ya wananchi wa eneo hilo.

(ii) Kituo kinatakiwa kiongeze thamani ya uchumi wa wananchi wa enelo usika. Ni vizuri ionekane tofauti kabla na baada ya kuanzishwa kituo.

(iii) Shughuli zote zitakazoendeshwa kituoni hapo ziwe ni zinafuata Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

(iv) Uhusishwaji wa wananchi, ambao ni watanzania wenyewe na vilevile kuboresha ushirikishwaji na mahusiano katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

(v) Kituokinalenga kuchangia juhudi za kumwezesha mtanzania kiuchumi na kuongeza kasi ya ukuaji kupitia kwa wananchi.

(vi) Ushirikishaji na utekelezaji wa shughuli za kituo utafanywa chini ya makubaliano ya kimkataba (MOU) ili kuweka bayana majukumu mbalimbali.


## 12.0. MUUNDO WA UTAWALA WA KITUO

Muundo wa utawala wa kituo utakuwa na ngazi tatu za usimamizi. Kituo kikianzishwa na mkoa kitasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa na kikianzishwa na Halmashauri kitasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Vilevile kutakuwa na Kamati ya Ushauri ambayo itakuwa ni kamati ya mashauriano ya Mkoa au Wilaya. Kwa ujumla vituo hivi vitasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa na Mkurugenzi wa Halmashauri ambao watakuwa na majukumu yafauatayo:

(i) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Halmashauri husika ndio itakuwa chombo chenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kituo cha Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

(ii) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Halmashauri husika itatoa taarifa za utekelezaji wa Kituo kwenye kamati ya mashauriano ya Mkoa au Wilaya .

(iii) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Halmashauri husika, itakuwa na jukumu la kutengeneza mfumo wa usimamizi wa kituo.




***Mchoro 3: Muundo wa Utawala wa Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi***

**MAJUKUMU YA TAASISI ZINAZOHUSIKA NA UTEKELEZAJI WA KITUO**

**12.1. OFISI YA MKUU WA MKOA NA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA**

i. Itakuwa mmiliki wa Kituo;

ii. Itasimamia uendeshaji wa Kituo;

iii. Itaweka na kudumisha kumbukumbu zinazohusiana na uendeshaji wa Kituo;

iv. Kubuni vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuendesha kituo;

v. Itaandaa mwongozo wa uendeshaji wa Kituo ama kuuboresha kwa kushirikiana na wadau

vi. Itatangaza huduma za kituo kwa wananchi;

vii. Itaandaa mpango kazi kwa kila mwaka kuutengea bajeti na kuuwasilisha katika kamati ya mashauriano ya Mkoa au Wilaya;

viii. Itaandaa ankara za kuombea mchango kwa taasisi zinatoa huduma ndani ya kituo kwa viwango vitakavyoridhiwa na taasisi hizo;

ix. Itaandaa ripoti ya fedha na kushiriki na taasisi katika Kituo;

x. Itaandaa taarifa ya Kituo na kuiwasilisha ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

xi. Itaratibu upatikanaji ama uteuzi wa wajumbe wa kamati ya ushauri;

xii. Itaandaa nyaraka zitakazojadiliwa katika vikao vya kamati ya mashauriano ya Mkoa au Wilaya;

xiii. Itapanga ratiba ya vikao vya ushauri, kuandaa ajenda za vikao, kutunza kumbukumbu zote zinazohusiana na uendeshaji wa vikao;

xiv. Itakuwa Katibu wa Kamati ya ushauri wa kuendesha Kituo;

xv. Itafuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao; na

xvi. Itaitisha vikao kila robo mwaka na taasisi zinazotoa huduma ndani ya kituo.

### 12.2. KAMATI YA MASHAURIANO YA MKOA AU WILAYA

Majukumu ya Kamati ya mashauriano katika kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi yatakuwa kama ifuatavyo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu;

ii. Kupanga na kushauri mipango na mikakati itakayosaidia kuboresha na kukuza huduma za kituo; na

iii. Kupokea taarifa za kila robo mwaka za kituo, kuzijadili na kuzitolea maamuzi.

### 12.3. MAJUKUMU YATAASISI ZINAZOTOA HUDUMA KWENYE KITUO

Majukumu ya watoa huduma yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kusaini daftari la mahudhurio kwa kila siku za kazi asubuhi na Jioni na endapo watatoka nje ya ofisi ndani ya masaa ya kazi mfano kutembelea wateja;

ii. Kufungua ofisi na kutoa huduma kwa wateja ndani ya siku za kazi (Jumatatu hadi Ijumaa) kuanzia 2:00 hadi 10:00 jioni;

iii. Kutoa huduma husika kama ambavyo Taasisi hiyo ilivyopewa dhamana na sheria iliyoianzisha.

iv. Kushiriki katika uchangiaji wa huduma za msingi za uendeshaji wa Kituo kama Umeme, Maji, Matengenezo madogo madogo ya miundombiu,Usafi nk

v. Kutangaza kituo kwa wananchi; na

vi. Kutoa taarifa za utendaji wa ofisi kwa kila Mwisho wa Mwezi, kila robo Mwaka na kila mwishoni mwa mwaka na kuiwasilisha kwa msimamizi wa kituo.

vii. Kuingia makubaliano ya kimkataba na Mkoa au Halmashauri ya Wilaya kwa ajili kuhakikisha kwamba kituo kinafikia malengo.

## 13.0. UTARATIBU WA KUGHARAMIA KITUO

Gharama za kuendesha Kituo kama vile Umeme, Maji, Usafi, Ulinzi, Matengenezo madogo madogo ya mara kwa mara ya Kituo yatafanywa na Taasisi zinazotoa huduma ndani ya Kituo. Aidha Msimamizi wa kituo atawajibika kuratibu zoezi zima la kufahamu gharama za watoa huduma, Uchangiaji na Ulipaji ili kuhakikisha kuwa huduma hizi zinapatikana muda wote ama pale itakapobidi. Gharama za uihishaji wa jengo zitafanywa na Halashauri husika.

## 14.0. VYANZO VYA MAPATO KWA KITUO

Msimamizi wa kituo atatakiwa kusimamia vyanzo vingine vya mapato nje ya michango toka kwa taasisi zinatoa huduma ndani ya Kituo. Mapato yatakayotokana na shughuli yoyote katika kituo yatawekwa kwenye akaunti na yatatumika kwa ajili ya kuongeza thamani ya utoaji wa huduma ndani ya kituo, pamoja na shughuli nyingine ambazo zitaonekana zinafaa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

## 15.0. MATUMIZI YA FEDHA ZA KITUO

Msimamizi wa Kituo atasimamia mapato na matumizi kulingana na sheria ya fedha za umma, aidha, masuala yote ya manunuzi ya Umma yatafuata sheria ya manunuzi ya umma.Pamoja na kufanya yafuatayo:-

i. Kufungua akaunti maalumu kwa ajili ya kituo na kuisimamia
ii. Kuwabainisha watoa huduma na kuandaa bajeti ya matumizi
iii. Kuandaa ankra za kuombea michango na kuzisamabaza kwa wahusika
iv. Kukusanya pesa za michango na kutoa stakabadhi
v. Kuwalipa watoa huduma kulingana na sheria zilizopo
vi. Kufanya suluhu ya mapato na matumizi
vii. Kuandaa taarifa ya mapato na matumizi na kuiwasilisha katika mikutano.

## 16.0. UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 16.1. UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na Tathmini utafanyika katika ngazi zote zinazoendesha shughuli za Kituo. Ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa shughuli za kituo utafanyika katika vipindi vya robo mwaka na kutoa taarifa za utekelezaji katika kila ngazi.

### 16.2. TATHMINI YA KITUO KIMAKUNDI

Tathmini ya Kituo kuhusu walengwa ambayo italenga kuona kama kituo kimesaidia kubadilisha hali ya uchumi kwa wajasiriamali, taasisi Mtoa Huduma na Msimamizi wa Kituo.Tathmini ya Kituo chenyewe ambayo inalenga kupanua wigo, ubora na ufanisi wa kituo pamoja na kuendeleza huduma zinazotolewa. Hii itajumuisha wadau wote wa kituo katika eneo litakalohusika na tathmini hiyo. Tathmini hii itafanyika kila baada ya mwaka mmoja na itaangalia viashiria vifuatavyo:

i. Idadi ya Viwanda vilivyoongezeka;
ii. Idadi ya walionufaika kijinsia;
iii. Pato kwa wananchi;
iv. Kiwango cha umaskini;
v. Ajira;
vi. Shughuli za kiuchumi;
vii. Idadi ya biashara ndogo zilizonufaika;
viii. Idadi ya biashara ndogo zilizounganishwa kwenye taasisi zingine za fedha ama huduma nyinginezo;
ix. Mikopo iliyotolewa kisekta kwa idadi na thamani kwa mfano kilimo, mifugo, viwanda n.k; na
x. Uelewa wa masuala ya fedha na elimu ya ujasirimali.

## 17.0. KITUO CHA MFANO MKOANI SHINYANGA, WILAYA YA KAHAMA

### 17.1. HISTORIA YA HALMASHAURI YA KAHAMA

Halmashauri ya mji wa Kahama ilianzishwa tarehe 17 Juni, 2011 chini ya kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa No. 8 ya 1982. Eneo lake la kijiografia linafanya kuwa makutano yanayounganisha barabara ya Mji wa Kahama, nchi za Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Uganda upande wa magharibi na sehemu ya Kaskazini inapakana na mkoa wa Geita. Wakati, upande wa Mashariki inapakana na mkoa wa Tabora. Halmashauri ya mji wa Kahama ina ukubwa wa eneo la kilomita 1520.2 (hekta 152,016.1) ambazo hekta 45,834.5 hutumiwa kwa ajili ya makazi na hekta 106,181.6 kwa ajili ya shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kilimo na ufugaji;

Halmashauri ya mji wa Kahama ina idadi ya watu wapatao 242,208 miongoni mwao 117,498 wanaume na 124,710 wanawake. Kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu ni asilimia 3.7. Kiwango

hicho kikubwa cha ukuaji kinasababishwa na uhamiaji wa watu badala ya kuongezeka kwa kuzaliana. Halmashauri ya mji wa Kahama ina idadi ya kaya 49,436 zenye wastani wa familia ya watu 5.

Halmashauri ya mji wa Kahama ni Kituo kikubwa cha biashara ambacho kimetokana na kuwepo kwa Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi ambao umekuwa ni chanzo cha ajira, ukuaji wa teknolojia ya uchakataji wa dhahabu na vilevile ni soko la bidhaa zinazozalishwa na wananchi wa Kahama na maeneo ya jirani.

Katika ukusanyaji wa mapato, Halmashauri ya mji wa Kahama ni ya pili katika ukusanyaji wa Mapato baada ya Halmashauri ya wialaya ya Kinondoni kwa takwimu za mwaka 2017/18;

Vilevile, Halmashauri ya mji wa Kahama ina fursa nyingi za uwekezaji. Fursa hizo ni pamoja na Uchimbaji wa Madini, biashara za hoteli, masoko mbalimbali, viwanda vikubwa na vidogo, sekta ya nyumba na makazi, shughuli za kilimo, mifugo na Ujasiriamali.

Katika Halmshauri hii kuna Taasisi za fedha zipatazo 14 zilizojikita katika utoaji wa huduma mbalimbali za kifedha ambapo uwepo wa Taasisi hizo za fedha inadhihirisha kuwa, Kahama ina idadi kubwa ya wananchi wanaojihusisha na uzalishaji unaosababisha kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa vyanzo vya mapato. Halmashauri hii vilevile, imetenga maeneo ya biashara kwa ajili ya wamachinga, ambao wamepewa maeneo ya kujenga vibanda vya muda vya biashara na wameshawishiwa kuanzisha Chama cha Ushirika ambayo ibapatiwa mikopo kwenye mapato ya Halmashauri. Halmashauri imetenga eneo la ekari 15,000 kwa jili ya kilimo cha Biashara, ambapo eneo hilo limekwisha pimwa na kufanyiwa utafiti kwa ajili ya maandalizi ya kilimo.

Mama Lishe pia wamejengewa majengo ya kisasa kabisa na Halmashauri ili kufanya biashara zao katika ubora unaotakiwa. Majengo ya mama Lishe yanachukuwa wapishi 50 na wateja wa chakula 2,500 kwa wakati mmoja.

### 17.2. MCHAKATO WA UANZISHWAJI WA KITUO CHA KAHAMA

Baada ya Baraza la Uwezeshaji kupokea maagizo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu liliwasiliana na Uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Shinyanga kwa ajili ya kupata eneo ambalo kituo hicho kitaanzanishwa. Kufikia mwezi wa Oktoba, 2018 Baraza lilikabidhiwa Jengo lenye Vyumba 22 lililoko katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, barabara ya Tabora kwa ajili kuanzisha Kituo hicho.

Baraza lilifanya mawasiliano na Taasisi mbalimbali ambazo zina majukumu ya kusaidia maeneo muhimu kama vile urasimishaji wa biashara, mafunzo na ujuzi mbalimbali, ufundi, huduma za upatikanaji wa mitaji, ushirika na vikundi, hifadhi ya jamii na teknolojia ya uzalishaji bidhaa mbalimbali. Taasisi 22 zilikubali kushirikiana na Baraza kuanzisha kituo hiki ambacho ni kituo kinachotoa huduma kama ilivyoelezwa hapo juu. Taasisi zilizopo katika kituo hicho ni SIDO,

TCCIA, BRELA, TANTRADE, GS1, TBS, NHIF, NSSF, NBC, TRA, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF), AGITIF, Mfuko wa Vijana, Mfuko wa Wanawake, Chuo Kikuu Huria, MKURABITA, SELF Micro finance, PASS Trust fund, VETA, Shirikisho la VICOBA Tanzania (VICOBA FETA), Taasisi ya VICOBA vya kidini (Inter-Religious VICOBA) na Tanzania Informal Microfinance Association of Practioners (TIMAP).

Kituo cha Kahama kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri MKuu (Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu) mnamo tarehe 18 Novemba 2018. Tangu kuzinduliwa kituo kimetembelewa na takriban wananchi **5748**. Kwa wastani kituo kinatembelewa na watu 100 kwa siku. Mrejesho tunaoupata kutoka kwa wananchi wa Kahama na wale wanaotembelea kituo kutoka mikoa ya jirani, ni kwamba wananchi wamefurahia na kufaidika sana na huduma za kituo.

### 17.3. USIMAMIZI WA KITUO CHA KAHAMA

Muundo wa Utawala na usimamizi wa kituo cha Kahama kwa kiasi kikubwa umefuata mwongozo huu. Lakini kwa kuwa ni kituo cha mfano na cha kuanzia Baraza linasimamia kwa karibu na linapata taarifa za kila mwezi kuhusu uendeshaji na maendeleo ya kituo.

### 17.4. TAASISI ZINAZOSHIRIKI NDANI YA KITUO CHA KAHAMA

Orodha ya Taasisi zilizoshiriki kuanzisha kituo cha Kahama ni kama ifuatavyo:-

| Na | Jina la Taasisi | Huduma inayotolewa |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) | Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji na kuratibu uendeshaji wa Kituo |
| 2 | Shirikisho la VICOBA Tanzania (VICOBA FETA) | Uratibu wa Vikundi na Uhamasishaji wa Kuweka Akiba |
| 3 | Taasisi ya VICOBA vya kidini (IR-VICOBA), | Uratibu wa Vikundi Vya Kidini vya akiba na mikopo na Uhamasishaji wa Kuweka Akiba |
| 4 | Tanzania Informal Microfinance Association of Practioners (TIMAP) | Uratibu wa Vikundi na Uhamasishaji wa Kuweka Akiba |
| 5 | Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) | Kutoa huduma za fedha,Mafunzo, Uendelezwaji wa Teknolojia na Ufundi |

| Na | Jina la Taasisi | Huduma inayotolewa |
|---|---|---|
| 6 | TBS/TFDA/BRELA | Urasimishaji wa Biashara, viwango vya ubora |
| 7 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) | Kuratibu, kusimamia, Kuwezesha, Kukuza na kutoa elimu ya ufundi na mafunzo Tanzania |
| 8 | Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) | Kuamsha na kuchochea umma wa watanzania kuwa na ari ya kuanzisha na kuendesha miradi ya maendeleo katika misingi ya kujitegemea na kujiajiri kwa kutoa mikopo na kujengea uwezo Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu (PWDs). |
| 9 | Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF) | Utekelezaji wa Sera ya Serikali kuhusu upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogowadogo kwa wakati unaofaa na kwa bei nafuu. |
| 10 | PASS TRUST FUND | Kuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara katika sekta zinazohusika kwa kutoa dhamana za Mikopo na elimu ya maendeleo ya biashara. |
| 11 | Mpango Wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) | Kuwawezesha wamiliki wa rasilimali ardhi na biashara kushiriki katika uchumi rasmi unaosimamiwa na utawala wa sheria. Hii ni pamoja na kuzitumia mali zao zilizokwisha rasimishwa kama dhamana katika kupata mikopo na fursa zinginezo zilizoko katika uchumi wa soko.<br><br>Walengwa wa MKURABITA ni wananchi wa mijini na vijijini wanaomiliki rasilimali nje ya mfumo unaotambulika kisheria na wanaoendesha biashara bila kukuidhi matakwa ya kisheria kwani rasilimali na biashara zinazomilikiwa na kuendeshwa nje ya mfumo rasmi haziwapi fursa wamiliki wake ya kujiongezea mitaji na kuingia katika uchumi wa soko |
| 12 | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | Kutoa elimu na kuimarisha ulipaji wa kodi wa hiari |

| Na | Jina la Taasisi | Huduma inayotolewa |
|---|---|---|
| 13 | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) | Kutoa mikopo yenye masharti nafuu hasa kwa wanawake wasio na vigezo au sifa za kukopesheka katika taasisi za fedha ili waweze kujikwamua kiuchumi na kupambana na Changamoto mbalimbali zinazowakabili kulingana na nafasi yao katika familia na jamii |
| 14 | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Uendelezaji wa Biashara (TANTRADE) | Huduma za Masoko na uendelezwaji wa Biashara |
| 15 | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) | Kuwawezesha vijana wote nchini (Tanzania Bara) kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha au kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali |
| 16 | SELF Microfinance Fund | (i) Kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali wadogo kupitia Asasi ndogo na za Kati za kifedha.<br>(ii) Kujenga uwezo wa Asasi Ndogo na za Kati kwa njia ya mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuwezesha Asasi hizi kujiendesha na kutoa huduma bora na endelevu kwa wananchi walengwa wa Mfuko.<br>(iii) Kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji kwa tija, ikiwa ni pamoja na kuwekeza mikopo hiyo vizuri, na hatimaye waondokane na umasikini |
| 17 | GSI Tanzania Limited | Kuwezesha biashara na kutoa msimbomilia kutoa huduma ya ufuatiliaji (traceability) wa bidhaa kutoka kwa mzalishaji hadi kufika kwa mlaji na ili zipate huongeza nafasi ya kupenya kwenye masoko ya ndani, kikanda na kimataifa, na hurahisisha utambuzi wa bidhaa hizo. |
| 18 | Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) | Kuwaunganisha Wajasiriamali wa biashara, viwanda na wakulima |

| Na | Jina la Taasisi | Huduma inayotolewa |
|---|---|---|
| 19 | Benki ya Taifa ya Biashara | Kufungua akaunti za vikundi kutoa huduma za kupokea pesa kwa wanufaika wa Mfuko wa NHIF, NSSF, Chuo kikuu huria cha Tanzania na wadau wengine |
| 20 | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) | Kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanapata huduma bora za Afya |
| 21 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii (NSSF) | Huduma za Hifadhi za Jamii |
| 22 | Chumba cha wazi kikubwa | Kutoa Mafunzo |